

# KUZURU MAKABURI

Kimeandikwa na:

**Sayyid Abdur-Rahim al-Musawi**

Kimetarjumiwa na:

**Hemedi Lubumba Selemani**

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:  
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 427 - 65 - 9**

Kimeandikwa na:  
**Sayyid Abdur-Rahim al-Musawi**

Kimetarjumiwa na:  
**Hemedi Lubumba Selemani**

Kimehaririwa na:  
**Ustadh Abdallah Mohamed**

Kimepangwa katika Kompyuta na:  
**Ukhti Pili Rajab**

Toleo la kwanza: Juni, 2008  
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:  
**Al-Itrah Foundation**  
P. O. Box 19701. Dar es Salaam, Tanzania  
Simu: +255 22 2110640  
Simu/Fax: +255 22 2127555  
Email: [alitrah@raha.com](mailto:alitrah@raha.com)  
Website: [www.alitrah.org](http://www.alitrah.org)  
Online: [www.alitrah.info](http://www.alitrah.info)

# YALIYOMO

Neno la Jumuiya.....	2
Kuzuru makaburi.....	4
Mazingatio na kuwaidhika.....	4
Kujikumbusha Akhera na kuipa nyongo dunia.....	6
Kuotesha hisia za mapenzi na huruma ya dhati.....	6
Mawahabi na suala la kuzuru makaburi la mtukufu Mtume s.a.w.w.....	19
Muhtasari wa uchunguzi.....	33



## Neno la Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: "Ziyaratu'l-Kubur" Kilichoandikwa na: **Sayyid Abdur-Rahim al-Musawi**

Sisi tumekiita: "Kuzuru makaburi."

Kuzuru makaburu ni desturi ambayo ilikuwepo tangu wakati wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Na wakati wa makhalfa na maimamu (a.s.) walien-deleza desturi hii, mpaka mwanzoni mwa karne ya 13 A.H. yalipozuka madhehebu ya Wahhabi, ndipo masheikh wa kiwahhabi wakaanza kuzunguka katika miji ya Waislamu na kuwakataza Waislamu kuzuru makaburi, huku wakisema ni shirik, bid'a na haramu.

Masheikh hawa wa kiwahhabi waliilazimisha itikadi yao hii kwa Waislamu, na hatimaye wakafikia kuyavunja makaburi ya wanachuoni wa Kiislamu na wajukuu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) pale *Janatu'l-Baqi* (Madina) katika mwaka wa 1343 A.H., na makaburi ya *Janatu'l-Muala* (Makka). Hali hii imeendelea mpaka imefika huku kwetu Afika ya Mashiriki, ziko taarifa kutoka sehemu mbali mbali za eneo hili la Afrika za kuvunjwa kwa makaburi ya Waislamu kwa amri ya masheikh wa kiwahhabi.


Kutokana na hali hii mwandishi wa kitabu hiki ameamua kuiangalia upya historia ya Uislamu na kutoa dalili katika Qur'an Tukufu na Sunna na akaonesha kwa uwazi kabisa kwamba kuzuru makaburi ni desturi iliyokuwepo tangu zama za Mtukufu Mtume (s. a. w.w.). Na mwenendo

huo ukafuatwa na makhalifa na masahaba baada ya Mtume. Kwa hiyo kuzuru makaburi sio shirk wala sio haram wala sio bid'a kama wanavyoitakidi kimakosa masheikh hawa wa kiwahhabi.


Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya '**Al-Itrah Foundation**' imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwashudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, **Hemedi Lubumba Selemani** kwa kukubali jukumu hili la kukifanya tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

**Mchapishaji:**  
**Al-Itrah Foundation**  
**S. L. P. 19701**  
**Dar-es-Salaam, Tanzania.**



F



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## Kuzuru Makaburi

---

### NENO LA JUMUIYA

Hakika mirathi ya Ahlul-Baiti ambayo imehifadhiwa na Kambi yao na wafiasi wao dhidi ya upotovu inaonyesha Kambi iliyokusanya aina mbalimbali za taaluma za kiislamu.

Kambi hii imeweza kulea nafsi mbalimbali zilizo tayari kunywa kutoka kwenye chemchemu hiyo, na kuupa umma wa kiislamu wanachuoni wakubwa wenyе kufuata nyayo za ujumbe wa Ahlul-Bait.

Wanachuoni wamekusanya vidodosa na maswali mbalimbali ya madhehebu na mitazamo tofauti ya kifikira kuanzia ndani ya desturi ya kiislamu hadi nje ya desturi hiyo, huku wao wakitoa majibu na utatuzi makini juu ya maswali hayo ndani ya karne zote.

Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Baiti imefanya hima kuteta matukufu ya ujumbe wa Uislamu na ukweli wake ambao umechafuliwa na makundi, madhehebu na wanaharakati mbalimbali wenyе chuki na Uislamu.

Jumuiya imefata nyayo za Ahlul-Baiti na za wafasi wa kambi yao njema ambayo imefanya hima kujibu madai yenyе kuendelea na daima ikajaribu kubaki ndani ya msitari wa mapambano kwa kiwango kinachohitajika ndani ya kila zama.

Hakika uzoefu ambao umehifadhiwa ndani ya vitabu vya wanachuoni wa Kambi ya Ahlul-Baiti katika dhamira hii ni wa aina ya pekee, kwa sababu una akiba ya kielimu inayotegemea akili na hoja, huku ukijiepusha na matamanio na upendeleo uliokatazwa.

Unazungumza na wasomi na wanafikra wenyе fani maalumu, mazungumzo ambayo yanakubalika kiakili na yanapokewa na maumbile yaliyo salama.

## Kuzuru Makaburi

Jaribio hili la Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul-Baiti limekuja kuwapa watafuta ukweli hatua mpya ya uzoefu wa thamani katika ulingo wa mazungumzo na maswali na kujibu hoja za utata zilizotolewa zama zilizopita au zinazotolewa leo kwa njia ya Tovuti, na hasa kwa kupewa nguvu na baadhi ya duru zenyenye chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Ikijiepusha na uchochezi uliokatazwa, na ni zenyenye kuhangaikia kuzishauri akili zenyenye kufikiria na nafsi zenyenye kutafuta haki, ili ziweze kufikia kwenye haki ambayo inatolewa na Kambi ya Ahlul-Baiti ulimwengu mzima, ndani ya zama ambazo akili inaerevuka na nafsi na roho zinaboreka kwa kasi ya pekee.

Ni lazima tugusie kuwa mfululizo huu wa tafiti hizi umeandaliwa na Kamati maalumu toka jopo la wanachuoni watukufu, hivyo tunatoa shukurani njema kwa hawa wote na kwa wasomi na wahakiki kwa kila mmoja mionganoni mwao kupitia sehemu ya tafiti hizi na kutoa mchango wao wa thamani kuhusu tafiti hizi.

Na sote tunategemea na kutaraji kuwa tutakuwa tumetoa kile tulichokiwaza katika juhudini za kutekeleza baadhi ya wajibu tulionao mbele ya ujumbe wa Mtukufu Mola wetu Mlezi ambaye alimtuma Mtume Wake na uongofu na dini ya haki ili aipe ushindi dhidi ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.

### **JUMUIYA YA KIMATAIFA YA AHLUL-BAITI KITENGO CHA UTAMADUNI**

## Kuzuru Makaburi

---

### KUZURU MAKABURI

Hakika kitendo cha kuzuru makaburi na kuwajali wafu ni mionganoni mwa vitendo vilivyozeleka ndani ya historia ya jamii ya wanadamu, na yule atakayefuatilia atakuta kitendo hicho hakihuji jamii ya kidini tu, wala Waislamu tu, bali ni kitendo wanachokijali watu wa jamii zote bila kujali tofauti zao za kimwenendo na kiimani.

Hakika msukumo unaompelekeea mwanadamu kuwaheshimu wafu na kutilia muhimu kuzuru makaburi unatokana na faida nyingi anazozipata kutoka kwenye kitendo hiki, ambazo ni kipawa halisi katika kiwango cha mtu mmojammoja na kijamii kwa jumla, kwa ajili hiyo ndio maana mataifa mbalimbali yakawa yanakijali.

Sheria tukufu imeelekeza mtazamo wa Waislamu kwenye umuhimu wa kuzuru makaburi, hivyo ikahimiza kufanya hivyo sehemu zaidi ya moja, ili yaweze kutimia baadhi ya malengo ya kimalezi ambayo faida zake zinarejea kwa mtu mmoja mmoja na jamii nzima kwa pamoja.

Tutatoa muhtasari wa baadhi ya faida hizo kama ifuatavyo:

#### Mazingatio na kuwaidhika

Kitendo cha kuzuru makaburi hutengeneza njia ya kuwaidhika na kupata mazingatio, kiasi kwamba mwenye kuzuru makaburi anajua kuwa vyovyste vile maisha yake yatakavyorefuka lakini mwisho wake ni kutoweka, hakika hisia hii yenye tu inakuwa ni kizuizi kinachomzuia kuzama ndani ya machafu, na hivyo Hadithi iliyopatikana kutoka kwa mtukufu Mtume (s.a.w.w.) imehimiza sana faida hii ya kuzuru, kwani imepokewa kauli yake (s.a.w.w.): “Nilikuwa nimewakatazeni kuyazuru makaburi, basi sasa yazuruni, kwani ndani ya hilo mna mazingatio.”<sup>1</sup>

<sup>1</sup> *Al-Mustadrak* cha Hakimu 1: 375, kitabu cha majeneza katika kuyazuru makaburi.

## Kuzuru Makaburi

Wala mazingatio ya kuzuru makaburi hayakomei kwenye kuyazuru makaburi ya mawalii na wachamungu tu, bali tunaikuta Qur'an Tukufu inatuelekeza maeneo yenyе mazingatio, yakiwemo hata kuzuru makaburi ya watu jeuri na waovu, kwani katika kuyazuru kuna mazingatio na kuwaидhika kamili. Mwenyezi Mungu amesema kuhusu Firauni:

﴿فَالْيَوْمَ نُنَحِّيَكَ بِبَدْنَكَ لِتَكُونَ لَمَنْ حَلَفَكَ إِيمَانَهُ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ﴾

عَنْ إِيمَانِنَا لَغَفْلُونَ ﴿٤٦﴾

**“Basi leo tutakuokoa kwa mwili wako ili uwe dalili kwa ajili ya wanumya yako. Na kwa kweli watu wengi wameghafilika na Aya zetu.”**

**Yunus: 92.**

Hivyo Mwenyezi Mungu kwa utashi wake akaufanya mwili wa Firauni kuwa mzoga uliotulia usiyokuwa na harakati yoyote, hali alikuwa anamili-ki uwezo wa aina mbalimbali mpaka kaumu yake ikadhani kuwa hatokufa.

Hivyo Aya ina wito wa waziwazi kwa Waisrael na vizazi vijavyo ikiwata-ka walizuru kaburi la Firauni ili washuhudie mwisho ambao Firauni ali-ishia, na watakaoishia watu mfano wake.

Az-Zamakhshari amesema ndani ya *Tafsir* yake kuwa: “Pamoja na ukub-wa wake na kiburi cha ufalme wake lakini mwisho wake ni kama mnayoona, kwa sababu ya kumuasi Mola wake Mlezi aliyetukuka, hivyo mnad-hania itakuwaje kwa mwagine? Au ili uwe funzo watakalojifunza mataifa baada yako, hivyo watakaposikia hali yako na dharau yako juu ya Mwenyezi Mungu wasijipe ujasiri kama ulivyojipa ujasiri kwake.”<sup>2</sup>

Hivyo hekima ya kumbakisha Firauni ni ili watu wamzuru, na ziara yenyeewe kama ilivyo hutoa mazingatio na kuwaидhika.

<sup>2</sup> *Al-Kash-shafu* cha Az-Zamakhshari 2: 369.

## Kuzuru Makaburi

### **Kujikumbusha Akhera na kuipa nyongo dunia**

Kitendo cha kuzuru makaburi kinasaidia kukomaza imani ya kuwepo Siku ya mwisho, imani ambayo ni msingi mionganoni mwa misingi ya dini, hivyo mwanadamu atakapoamini kuwa baada ya leo kuna siku ambayo atahojiwawa juu ya yale aliyoyatenda na kuwa yeye hakuumbwa bila lengo, basi hisia hii ya kina ya Siku ya mwisho inamfanya mwanadamu awe na kusudio kwenye matendo yake, na hivyo kujiepusha kutenda shari na uharibifu, na kuelekea kutenda kheri ambayo lengo lake ni kutengeneza.

Hivyo hapa kitendo cha kuzuru makaburi kinakuwa njia ya kumlea mwanadamu mwislamu awe mwenye makusudio *chanya* katika vitendo vyake, pia kwenyewe kunaimarisha imani ya kuwepo Siku ya Mwisho, na kuzuia pupa ya kutaka kuzifikia haja za dunia yenyekutoweka hata kwa njia zisizokuwa za kisheria.

Faida hii ndio iliyoashiriwa ndani ya Hadithi iliyopokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.): “Nilikuwa nime-wakatazeni kuyazuru makaburi, basi sasa yazuruni, kwani yanafanya mtawe dhidi ya dunia na yanakumbusha Akhera.”<sup>3</sup>

### **Kuotesha hisia za mapenzi na huruma ya dhati**

Kuzuru makaburi kunapelekea kuzalika hisia za vitendo vya kheri na kupenda matendo mema, yamepatikana maelezo kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwa alisema: “Mimi nilikuwa nimewakatazeni kuyazuru makaburi, basi sasa yazuruni, ili huko kuyazuru kuwazidishieni kheri.”<sup>4</sup>

<sup>3</sup> *Sunan Ibnu Majah* 1: 501, mlango wa 47, Hadithi ya 1571.

<sup>4</sup> *Al-Mustadrak* cha Hakimu 1: 376, kitabu cha jeneza.

## Kuzuru Makaburi

Na ndani ya hadithi nyingine akasema: “.....Basi yazuruni; hakika kufanya hivyo kunalainisha moyo na yanayavujisha macho machozi na yanakumbusha Akhera, na wala msiseme maneno machafu.”<sup>5</sup>

Hivyo kilio kitokanacho na mapenzi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu huzalisha uhusiano mwema kati ya binadamu hai na binadamu mfu, na mahusiano ya mtu binafsi na jamii, na hapo hupatikana ulingano, kuhurumiana, mapenzi na wema kati ya watu, na hivyo haki kutolewa na amana kutekelezwa.

Hizi ni baadhi tu ya faida zinazotokana na kitendo cha kuyazuru makaburi, lakini tunachotaka kukichunguza katika suala hili ni ile ruhusa ya kisheria ya kuyazuru makaburi na uhusiano wake na imani, kupertia rai na misimamo ya wanachuoni wa madhehebu mbalimbali ya kiislamu juu ya suala hili. Hivyo uchunguzi juu ya ruhusa hii ya kisheria utatimia kwa kupertia mambo mbalimbali:

### **Kwanza: Maana ya kilugha**

Neno Ziara ndani ya lugha ya kiarabu humaanisha kutembelea na kuktana. Na kwa uframamu wa kijamii juu ya neno Ziara ni kumtembelea mwenye kutembelewa kwa ajili ya kumheshimu na kujiliwaza kwake.<sup>6</sup>

### **Pili: Dalili ya Qur'an juu ya Sheria ya kuzuru makaburi**

Hakika Mwenyezi Mungu alimkataza Mtume wake Muhammad (s.a.w.w.) kuswalia maiti ya mnafiki na kusimama juu ya kaburi lake kwa kusema:

---

<sup>5</sup> Chanzo kilichotangulia.

<sup>6</sup> *Al-Misbahu al-Munir*: 260.

## Kuzuru Makaburi

﴿ وَلَا تُصْلِّ عَلَىٰ أَحَدٍ مِّنْهُمْ مَاتَ أَبْدًا وَلَا تَقْعُمْ عَلَىٰ قَبْرَهُ إِنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَمَا تُوْلَى وَهُمْ فَسِقُوتٌ ﴾ ﴿٤٣﴾

**“Kamwe wala usimswalie ye yote akifa mi ongoni mwao, wala usisimame kaburini pake. Hakika wao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakafa hali ni wenye kuvunja amri.” Tawba: 84.**

Na muulizaji ana haki ya kuuliza ni ipi maana ya: Usisimame kaburini pake? Je, ni kusimama wakati ule wa kuzika tu, au ni wakati ule wa kuzika na wakati mwingine?

Jibu ni kuwa Aya inafanyika kwa sentensi mbili:

Ya kwanza: “Kamwe wala usimswalie ye yote akifa mi ongoni mwao,” na ya pili ni: “Wala usisimame kaburini pake.” Sentensi hii ya pili imeifuata sentensi iliyotangulia, na kila kinachothibiti kwenye kile kinachofuatwa, basi pia huthibiti kwenye hiki kinachofuata. Na tayari kinachofuatwa kimeshahushisha na sharti nalo ni “kamwe.”

Hivyo hili linalazimu sharti hili kuwa pia sharti la kinachofuata, na maana yake inakuwa: Kamwe usisimame kwenye kaburi la ye yote mi ongoni mwao. Kama ilivyokuwa kwa upande wa Swala.

Na tamko “Kamwe” linalokadirwa kwenye sentensi ya pili, hapo linafidisha uwezekano wa kitendo hiki kurudiwa, na kuto kana na hilo tunapata kuwa kusimama kaburini hakuhusu wakati ule wa kuzika tu.

Lakini mtu anaweza kupinga na kusema: Hakika tamko “Kamwe” linalokadirwa kwenye sentensi ya pili limekuja kuonyesha mjumuisho wa mifano halisi<sup>7</sup>.

<sup>7</sup> Mjumuisho wa mifano halisi: Humaanisha kuwa mifano yote inahusika na hukumu hiyo, hivyo neno hilo huja kuhusisha mifano yote bila kubagua. Hivyo hapo itamaanisha kuwa hukumu hiyo inahusu makaburi yote bila kubagua - **Mtarjumi.**

## Kuzuru Makaburi

Jibu: Hakika tamko “yejote” limeonyesha mjumuisho wa mifano halisi, na wala si tamko “Kamwe” kwa sababu lenyewe linaonyesha mjumuisho wa nyakati<sup>8</sup>.

Hivyo tunapata kuwa Mwenyezi Mungu anamkataza Mtume wake (s.a.w.w.) kumuombea mnafiki aina yoyote ya msamaha na rehema, sawa iwe baada ya Swala au dua yoyote. Na anamkataza kusimama kwa aina yoyote kaburini, sawa iwe wakati ule wa kuzika au baada yake.

Hivyo kinachofahamika hapo ni kuwa haya mambo mawili: Swala na kusimama kaburini yanaruhusiwa kutendewa muumini na wala hayaruhusiwi kutendewa mnafiki. Na hapo inathibiti ruhusa ya kulizuru kaburi la muumini na ruhusa ya kuisomea roho yake Qur’ani hata baada ya maelfu ya miaka.<sup>9</sup>

### **Tatu: Dalili ya riwaya juu ya uhalali wa kuyazuru makaburi**

Ama riwaya ambazo zimehimiza kuzuru makaburi na kuwaombea dua waliomo humo au kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya ziara, zipo katika makundi mawili:

#### **Kundi la Kwanza:**

Iliyopokewa kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w), kuwa alisema: “Hakuna mtu yeyote atakayelizuru kaburi la kipenzi chake, kisha akamtolea salamu na kukaa kwenye kaburi lake, ila ni lazima atamrudishia salamu na atamliwaza mpaka atakapoondoka kwake.”<sup>10</sup>

<sup>8</sup> Mjumuisho wa nyakati: Humaanisha kuwa hukumu hiyo ni ya nyakati zote, hivyo neno hilo huja kuhusisha nyakati zote bila kubagua. Hivyo hapo itamaanisha kuwa hukumu hiyo inahusu nyakati zote bila kubagua - **Mtarjumi**

<sup>9</sup> Rejea Ziyaratul-Kubur Ala Dhaw’ul-Kitabu Wasunnah: 127.

<sup>10</sup> *Al-Bayanu*: 520, ameipokea Sheikh Ad-Daylamiyu. *Kanzul-Ummal* 13: 656, hadithi ya 42601.

## Kuzuru Makaburi

Iliyopokewa kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kuwa alisema: "Hakuna mtu ye yote anayepita kwenye kaburi la mtu aliye kuwa anamjua duniani, kisha akamsalimia, ila ni lazima mtu yule atamjua na kumrudishia salamu."<sup>11</sup>

Pia imepokewa kutoka kwa Abu Huraira kuwa: Mtume (s.a.w.w.) alikwenda makaburini na kusema:

**"السلام عليكم دار قوم مؤمنين وإنما إنشاء الله بكم لاحقون"**

"Amani ikufikieni enyi watu wa makazi ya Waumini, nasi apendapo Mwenyezi Mungu tutafika huko."<sup>12</sup>

Imepokewa kutoka kwa Buraydah kuwa alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alikuwa anawafunza kuwa pindi watokapo kwenda makaburini mtu aseme:

**"السلام عليكم أهل الديار من المؤمنين وال المسلمين وإنما إنشاء الله بكم لاحقون نسأل الله لنا ولكلم العافية."**

"Amani iwafikie enyi watu wa makazi haya mionganoni mwa waumini na waisilamu, nasi apendapo Mwenyezi Mungu tutafika huko mliko ninyi. Namuomba Mwenyezi Mungu atupe afya sisi na ninyi pia."<sup>13</sup>

Imetoka kwa Aisha kuwa Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Mola wangu Mlezi ameniamuru niende Baqii nikawaombee msamaha." Nikasema, nitasemeje ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: Sema:

<sup>11</sup>. *Tahdhibus Tarikh Damash'qi* cha Ibnu Asakir 7: 292, chapa ya Beirut.

<sup>12</sup> *As-Sunan al-Kubra* cha Al-Bayhaqi 4: 131, Hadithi ya 7207.

<sup>13</sup> Ameipokea Muslim ndani ya *Sahih yake* 3: 65, kitabu cha jeneza, huku ikito-fautiana kidogo na ile ya Ibnu Majah, uhakiki wa Dr. Bashari 3: 78, kitabu cha majeneza, mlango wa 36, hadithi ya 1547. *Al-Muntaqa min Akh'barul-Mustafa* 2: 116.

## Kuzuru Makaburi

**"السلام على أهل الديار من المؤمنين والمسلمين يرحم الله  
المستقدمين والمستأخرين وإنما إنشاء الله بكم لا حقول"**

"Amani iwafikie watu wa makazi haya mionganini mwa waumini na waisilamu. Mwenyezi Mungu awarehemu waliyokwisha tangulia mionganini mwetu na hao watakaokuja baadaye, nasi apendapo Mwenyezi Mungu tutakutana nanyi."<sup>14</sup>

### Kundi la Pili:

Kundi hili linahimiza kuzuru makaburi baada ya kukataza kufanya hivyo, zaidi ya hapo linataja sababu na lengo la Mwekasheria kuweka ibada hii.

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) kuwa alisema: "Nilikuwa nimewakatazeni kuyazuru makaburi, basi sasa yazu-runu, kwani yanafanya mtawe dhidi ya Dunia na yanakumbusha Akhera."<sup>15</sup>

Mtume alilizuru kaburi la mama yake mzazi, hivyo akalia na kuwaliza waliyomzunguka....s Kisha akasema: "Nimemuomba Mola wangu Mlezi ruhusa ya kulizuru kaburi lake, na ameniruhusu, basi nanyi yazuruni makaburi kwani yatakukumbusheni kifo."<sup>16</sup>

Imepokewa kuwa Aisha alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu aliruhusu kuyazuru makaburi.<sup>17</sup>

<sup>14.</sup> *Sahih Muslim* 3: 64, mlango wa yanayosemwa wakati wa kuingia makaburini. *Sunan An-Nasai* 3: 76.

<sup>15</sup> *Sunan Ibnu Majah* 1: 114, milango ya majeneza.

<sup>16</sup> *Sahih Muslim* 3: 65, mlango wa Mtume kumuomba Mola wake Mlezi ruhusa ya kulizuru kaburi.

<sup>17</sup> *Sahih Abi Daud*: 2, kitabu cha majeneza, mlango wa kuyazuru makaburi, hadithi ya 1955.

## Kuzuru Makaburi

Kutokana na kundi hili inaonekana kuwa Mtume alikuwa keshakataza kuyazuru makaburi, lakini katazo la muda mfupi, kisha akaondoa katazo, na baada ya hapo akahimiza sana kuyazuru makaburi.

Inasemwa kuwa sababu ya kukatazwa kwa muda ni kwa kuwa Waislamu walikuwa wageni ndani ya Uislamu, hivyo wakawa wakiwalilia wafu wao kilio batili kinachowatoa kwenye sheria. Lakini pindi Uislamu ulipokomaa ndani ya nyoyo zao na wakazijua kanuni na sheria za Uislamu na huku makaburi yao yakiongezeka, kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtume akaondoa katazo hilo dhidi ya kuyazuru makaburi, kutokana na athari nzuri na matokeo mazuri yaliyomo humo.<sup>18</sup>

### Nne: Dalili ya kihistoria:

Mwenye kufuatilia sera ya Waislamu tangu zama za mwanzo, kabla na baada ya kifo cha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu ataikuta imesimamia kwenye kuyazuru makaburi, na ufuatao ni baadhi tu ya ushahidi wa kihistoria juu ya hilo:

Siku moja Marwan alikwenda akamkuta mtu ameweka uso wake juu ya kaburi akamshika shingo yake na kumwambia: “Je, unafahamu unachokifanya?” Akamgeukia kumbe ni Abu Ayyub Al-Ansari akamjibu: “Mimi nimemjia Mtume wa Mwenyezi Mungu na wala sikulija jiwe, nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: ‘Msililie dini kama mtawala wake ni mtu anayestahili lakini ililieni dini kama mtawala wake ni mtu asiyestahili<sup>19</sup>’.”

Hakika Fatima alikwenda kwenye kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akachukua gao la udongo wa kaburi na kuuweka juu ya macho yake huku akilia.<sup>20</sup>

Hakika bedui mmoja alikwenda kwenye kaburi la Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu, akajipaka kichwani udongo wa kaburi lake na kumse-

<sup>18</sup> Rejea Ziyaratul-quburi fil-Kitabi Wasunnah: 128.

<sup>19</sup>. Ameipokea Al-Hakimu ndani ya Al-Mustadrak 4: 515.

<sup>20</sup>. Kashful-Irtiyabu: 436, amenukuu kutoka kwenye Tuhfatu cha Ibnu Asakir.

## Kuzuru Makaburi

meza akisema: Na mionganini mwa yale uliyoteremshiwa ni “Na lau wan-gelikujia walipojihulumu nafsi zao...” Na mimi nimejidhulumu na nimekujia unionbee msamaha. Basi ikanadiwa kutoka kaburini: Hakika Mwenyezi Mungu amekusamehe. Na hili lilitokea mbele ya Ali, Kiongozi wa waumini.<sup>21</sup>

Hakika Bilal alikwenda kwenye kaburi la Mtukufu Mtume na akaanza kulia hapo huku akiusuga uso wake juu ya kaburi, ghafla wakaja Hasan na Husein akawakumbatia huku akiwabusu.<sup>22</sup>

Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Malikah kuwa Aisha alikwenda siku moja kutoka makaburini, nikamwambia: Ewe Mama wa Waumini umetoka wapi? Akasema: “Kwenye kaburi la kaka yangu Abdur-Rahmani.” Nikamwambia: Mtume si alikuwa amekataza kuyazuru? Akasema: “Ndiyo, alikuwa keshakataza kuyazuru makaburi, kisha baadaye aliamuru kuyazuru.”<sup>23</sup>

Na Ibnu At-Taymiyyah amethibitisha ruhusa ya kulizuru kaburi la Abubakr na Umar bin Al-Khattabi kwa kuwa Ibnu Umar aliyazuru. Akasema: “Salamu ya kumtolea Abu Bakr As-Swidiqi na Umar bin Al-Khattabi ni ileile ya kuyatolea makaburi mengine.”

Na Ibnu Umar alikuwa akimtolea salamu Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu na Sahaba zake wawili pindi atokapo safarini, alikuwa akisema: “Amani iwe juu yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Amani iwe juu yako ewe Abu Bakr. Amani iwe juu yako ewe baba yangu.” Kisha anaondoka. Na ndipo baadhi ya Wanazuoni wakaona kuwa hili linaruhusiwa kwa kuwafuata Sahaba radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao.<sup>24</sup>

<sup>21</sup> *Wafaul-Wafa* cha Samuhudi 2: 1361.

<sup>22</sup> *Usudul-Ghabah* 1: 208.

<sup>23</sup> *As-Sunan Al-Kubra* cha Al-Bayhaqi 4: 131, mlango wa 170, hadithi ya 7207.

<sup>24</sup> *Tambibi Zairul-Madinah*: 27, amenukuu kutoka kwenye *Al-Jawabu Al-Bahiru fi Ziyaratil-Maqabiri* cha Ibnu At-Taymiyyah: 60.

## Kuzuru Makaburi

Hivyo kwa mtazamo wa Qur'ani, Hadithi Tukufu na sera ya waislamu inathibiti ruhusa ya kuyazuru makaburi ya waumini kwa ujumla.

**Tano: Kutawassali kwenye kaburi la Mtume (s.a.w.w.)**

Na tunaweza kuthibitisha ruhusa ya kuzuru makaburi kupitia ruhusa ya kutawassali kupitia kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa kuzingatia Tawassuli ni ibada isiyokuwa na shaka, na mwanadamu Mwisilamu anaweza kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa njia hiyo. Na Qur'ani Tukufu imehimiza hilo ndani ya zaidi ya Aya moja, kwa muhtasari mionganoni mwake ni:

﴿ قَالُوا يَأَبَانَا أَسْتَغْفِرُ لَنَا ذُنُوبَنَا ﴾

**“Wakasema: Ewe baba yetu, tuombee msamaha kwa dhambi zetu, hakika sisi tulikuwa wenye makosa.” Yusuf: 97.**

Tunakuta wana wa Yakub wameomba msamaha kutoka kwa Yakub, lakini si kwa kuutenga uwezo wa Mwenyezi Mungu, bali wamemfanya Yakub kiungo katika kutafuta msamaha, kwa kuwa yeye ni mwenye ukuruba mno mbele ya Mwenyezi Mungu na mwenye jaha kwake.

Na hili liko wazi kupitia jibu la Yakub kwa wanawe:

﴿ قَالَ سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الْرَّحِيمُ ﴾

**“Akasema: Nitakuombeeni msamaha kwa Mola wangu Mlezi, kwani yeye ndiye Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu.” Yusuf: 98.**

Vilevile Hadithi Tukufu zimehimiza ruhusa ya kutawassali. Imepokewa kutoka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: “Alipofariki Fatima binti Asad, Mtume aliingia mahala alipofia akakaa upande wa kichwa chake akasema: Arabic txt “Mwenyezi Mungu akurehemu ewe mama yangu baada ya

## Kuzuru Makaburi

mama yangu.” Akataja sifa zake juu yake na kumvisha sanda kwa joho lake, kisha Mtume akamwita Usama bin Zaydi, Abu Ayyub Al-Ansari, Umar bin Al-Khattabi na kijana fulani mweusi ili wakachimbe kaburi.

Wakalichimba kaburi lake na walipofikia kuchimba mwanandani Mtume akaichimba hiyo ye ye mwenyewe kwa mkono wake na kuutoa mchanga kwa mkono wake. Alipomaliza akaingia kwenye mwanandani kisha akalala ndani yake na akasema:

**”الله الذى يحيى ويميت وهو حي لا يموت اغفر لامي فاطمة بنت أسد؛ ووسع عليها مدخلها بحق نبيك والأنبياء الذين قبله.“**

“Mwenyezi Mungu ndiye anayehuisha na kufisha, na ye ye yu hai wala hatokufa. Ewe Mwenyezi Mungu msamehe mama yangu mpendwa Fatima binti Asad na uyapanue makazi yake kwa haki ya Mtume wako na Manabii ambao wamepitaa kabla yangu.”<sup>25</sup>

Ama sera ya Waislamu kuhusu kutawassali iliendelea baada ya kifo cha Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu. Hivyo tunamkuta Abu Bakr baada ya kufariki Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema: “Ewe Muhammadi tutaje mbele ya Mola wako Mlezi na tuwe ndani ya kumbukumbu yako.”<sup>26</sup>

Ndani ya Sahih Bukhari imetajwa kuwa: Umar bin Al-Khattabi alikuwa kila wanapopatwa na ukame huomba mvua kupitia Abbas bin Abdul-Mutwalibi (r.a.) na kusema: “Ewe Mwenyezi Mungu tulikuwa tukitawasali kwako kupitia Mtume wetu na ukitupa mvua, basi sasa tunatawasali kwako kupitia ami ya Mtume wetu basi tupe mvua.” Bukhari amesema: Basi hupewa mvua.”<sup>27</sup>

<sup>25.</sup> *Kashful-Irtiyabi*: 312, amenukuu toka kwenye *Wafaul-Wafai* na *Ad-Duraru As-Saniyah*: 8.

<sup>26.</sup> *Ad-Duru As-Saniyyah fi radi Alal-Wahabiyyah*: 36.

<sup>27</sup> *Sahih Bukhari*: Mlango wa Sala ya kuomba mvua 2: 22, hadithi ya 947.

## Kuzuru Makaburi

Al-Mansuri Al-Abasiyyu alimuuliza Malik bin Anas – Imamu wa madhe-hebu ya Malik - kuhusu namna ya kumzuru Mtume (s.a.w.w.) na namna ya kutawasali kuititia yeye ... akamwambia Malik: “Ewe Abu Abdullah, nielekee Kibla niombe au nimwelekee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?”

Katika kumjibu Malik akasema: “Kwa nini unampa kisogo Mtume wakati yeye ndiyo njia yako na njia ya baba yako Adam Siku ya Kiyama? Bali mwelekee na umwombe akuombee na Mwenyezi Mungu atakubali maombi yako, kwani Mwenyezi Mungu anasema: “Na lau walipozidhulumu nafsi zao...”<sup>28</sup>

Hivyo ikiwa Tawassuli ni mionganoni mwa ibada zilizoruhusiwa kisheria na Waislamu walikuwa wakitawasali kuititia Mtukufu Mtume, Manabii na Wachamungu, basi kulizuru kaburi lake linajumuisha Tawassuli yake, au Tawassuli inatimia kwa njia ya kulizuru kaburi lake tukufu, kwa ajili ya kufuata sera za wema walijotangulia.

### Sita: Kulizuru Kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

Aya za Qur’ani na Hadithi Tukufu zinaamuru kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume na kuomba hapo dua, zaidi ya hapo ni Ijimai ya Waislamu wote wa sasa wakirithi kutoka kwa walijotangulia, tokea zama za Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu mpaka leo hii, na wala hutomkuta mtu anayekanusha kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume ila Muwahabi.

Ama ushahidi wa Qur’ani ni kuwa Mwenyezi Mungu amesema:

﴿ وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَآتَسْتَغْفِرُوا اللَّهَ وَآتَسْتَغْفِرَ لَهُمُ الرَّسُولُ ﴾

﴿ لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَابًا رَّحِيمًا ﴾

**“Na lau wangelikujia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, na Mtume akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu, Mwenye kupokea toba, Mwenye**

<sup>28</sup> Kutoka kwenye *Wafaul-Wafai* cha As-Samuhudi 2: 1376.

## Kuzuru Makaburi

**kurehemu.”*An-Nisai: 64.***

Kwa Aya hii Qur’ani Tukufu inawaamuru wenyе dhambi wahudhurie kwa Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu na wamuombe awaombee msama-ha, kwa sababu dua ya Mtukufu Mtume ni yenyе kujibiwa.

Wala Aya hii haikuwa mahususi kwa ajili ya zama za uhai wa Mtukufu Mtume tu na zama za kuwepo kwake kati ya watu, bali ndani ya Aya hiyo tunapata muhtasari wa hukumu jumuishi yenyе kuenea mpaka baada ya uhai wa Mtume (s.a.w.w.).

Kwa sababu Qur’ani imetamka wazi uhai wa Manabii na Mawalii kwenye maisha ya Barzakhi, na inawazingatia kuwa ni wenyе kuona na kusikia ndani ya ulimwengu huo. Zaidi ya hapo ni kuwa zimepatikana hadithi tukufu ambazo zimetamka wazi kuwa Malaika humfikishia hitimisho la Manabii (s.a.w.w.) salamu za anayemsalimu.<sup>29</sup>

Ndani ya *Sahih Sita* imepokewa kuwa: Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema: “Hapana ye yote atakayenisalimia isipokuwa Mwenyezi Mungu hunirudishia roho yangu mpaka nami nimrudishie salamu.”<sup>30</sup>

Na pia imepokewa kutoka kwake kuwa alisema: “Niombeenii rehma, kwani hakika rehma zenu hunifikia toka popote mtakapokuwa.”<sup>31</sup>

Na Abu Said As-Samuani amepokea kutoka kwa Ali bin Abu Twalib kuwa (a.s.) alisema: “Baada ya siku tatu tangu tulipomzika Mtume wa Mwenyezi Mungu alitujia bedui akajitupa juu ya kaburi la Mtume (s.a.w.w.) na kumwagia sehemu ya udongo wake juu ya kichwa chake na kusema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ulisema tukasikia kauli yako. Ukatuelimisha kuhusu Mwenyezi Mungu na tukaelimika kuhusu wewe, na mionganii mwa

29. Rejea *Ziyaratul-Kuburi Fil-Kitabi Wasunnah*: 129 na kurasa za baada yake.

30 -Rejea *Sunan Abu Daud* 1: 470 – 471, kitabu cha Hija, mlango wa kuyazuru makaburi

31 *At-Taji Al-Jamiu lil-Usuli fi Ahadithi Ar-Rasuli* 2: 189.

## Kuzuru Makaburi

yaliyoteremshwa ilikuwa ni: “Lau wangelikuijia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu.....” Na nimeshaidhulumu nafsi yangu na nimekuijia unionbee msamaha kwa Mola wangu Mlezi.”<sup>32</sup>

Kuanzia hapa inaruhusiwa kwa mwanadamu kusimama kwenye kaburi la Mtukufu Mtume baada ya kifo chake na kumuomba amuombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu, na kwa hili inathibiti ruhusa ya kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume kwa sababu hali yake halisi inamaanisha mwenye kuzuru kahudhuria kwa mwenye kufanyiwa ziara.

Ama Hadithi zinazopatikana ndani ya *Sahih Sita* kuhusu kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume ni nyingi sana, hapa tutafupisha kwa kutaja baadhi yake tu:

Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Umar kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema: “Atakayelizuru kaburi langu basi atalazimika kupata shufaa yangu.”<sup>33</sup>

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa alisema: “Yeyote atakayenijia kwa lengo la kunizuru na ikawa hakuna kingine kilichomfikisha kwangu ila kunizuru mimi tu, basi nitakuwa na wajibu wa kuwa mwombezi wake Siku ya Kiyama.”<sup>34</sup>

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa alisema: “Mwenye kuhiji bila kunizuru ameniepuka.”<sup>35</sup>

<sup>32</sup> *Al-Jawharu Al-Munadhamah* cha Ibnu Hajari. Na pia Samuhudi ameitaja ndani ya *Wafaul-Wafai* 2: 612, na Dahlani ndani ya *Ad-Duraru As-Saniyyah*: 21.

<sup>33</sup> *Al-Fiq’hu Alal-Madhahibi Al-Ar’baah* 1: 590, na Wanazuoni wa Madhehebu Manne wametowa fatuwa kulingana na hadithi hii, rejea kitabu *Wafaul-Wafai* 4: 1336.

<sup>34</sup> Kuhusu njia za upokezi wa hadithi hii na wapokezi wake, rejea *Shifau As-Suqami* cha Taqiyu Ad-Dini As-Sabkiyyu.: 3 – 11. na pia *Wafaul-Wafai* cha Samuhudi 4: 134.

<sup>35</sup> *Wafaul-Wafai* 4: 1342.

## Kuzuru Makaburi

Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa alisema: “Mwenye kuhiji kisha akalizuru kaburi langu baada ya kufa kwangu, atakuwa kama amenizuru katika zama za uhai wangu.”<sup>36</sup>

### Mawahabi na Suala la kuzuru Kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

Ibnu At-Taymiyyah na aliyemuata katika msimamo wake mkali, Muhammad bin Abddul-Wahhab katika risala ya pili, kwenye risala za Al-Hadiyat Sunniya, wametoa dalili juu ya uharamu wa kulizuru kaburi la Mtume kwa kutumia Hadithi iliyonukuliwa kutoka kwa Abu Huraira kuto-ka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.): “Haifungwi safari ila kwenda kwenye misikiti mitatu: msikiti wangu huu na msikiti wa Makka (Masjidul-haram) na msikiti wa Jerusalem (wa Aqsa).”<sup>37</sup>

Na Ibnu At-Taymiyyah akaongeza maneno kwenye Hadithi hii kwa kuse-ma: “Hadithi hii ni Sahih, Maimamu wameafikiana juu ya usahihi wake na juu ya kuifanyia kazi, hivyo laiti mtu akiweka nadhiri ya kusalia msikiti fulani au jengo fulani au acae humo kwa ajili ya Itikafu na asafiri kwenda msikiti usiyokuwa hiyo mitatu, basi kwa mujibu wa itifaki ya Maimamu nadhiri hiyo haiwi wajibu kwake.”<sup>38</sup>

Hamna shaka kuwa hadithi hii imo ndani ya *Sahih Sita*, na wala hapa hatuko kwenye mjadala juu ya njia yake ya upokezi, bali makusudio yetu ni kuangalia maana ya Hadithi hii.

<sup>36.</sup> *Wafaul-Wafai* 4: 1342.

<sup>37.</sup> *Sahih Muslim* 4: 126, kitabu cha Hija, mlango wa huwa haifungwi safari. Na Abu Daud ameitaja ndani ya *Sunani* yake 1: 469, kitabu cha Hija. Na An-Nasai ndani ya *Sunani* yake, pamoja na *Sharhu As-Suyutwi* 2: 37 – 38.

<sup>38.</sup> *Radu Alal-Akh'nai* cha Ibnu At-Taymiyyah

## Kuzuru Makaburi

Na hebu tufanye kuwa maelezo ya hadithi ni: "Haifungwi safari ila kwen-da kwenye misikiti mitatu." Ni thabiti kuwa "ila" kilugha ni nyenzo ya kuvua, na hivyo ni lazima kipatikane kilichovuliwa, na ni lazima kipam-banuliwe, na kwa kuwa hakipo kwenye maelezo basi ni lazima tukikadirie ndani ya maneno haya.

Na kabla hatujagusia vielelezo vilivyopo tunaweza kukadiria kilichovuli-wa kwa sura mbili:

Haifungwi safari kwenda kwenye msikiti wowote mionganoni mwa misikiti isipokuwa misikiti mitatu....

Haifungwi safari kwenda sehemu yoyote mionganoni mwa sehemu isipokuwa kwenye misikiti mitatu...

Hakika kuifahamu Hadithi hii na kuichunguza maana yake kunategemea moja ya makadirio haya mawili. Basi iwapo tutachagua kadirio la kwanza, maana ya Hadithi itakuwa ni kutokufungwa safari kwenda msikiti wowote isipokuwa misikiti ile mitatu, wala haitakusudia kutoruhusu kufungwa safari kwenda sehemu yoyote hata kama sehemu hiyo siyo msikiti.

Kwa hiyo katazo lililopo halimuhusu yule anayefunga safari kwa ajili ya kuwazuru manabii, maimamu watakasifu na wachamungu, kwa sababu maudhui inayozungumziwa ni ufungwaji wa safari za kuzuru misikiti kwa kuvua misikiti mitatu iliyotajwa. Ama anayefunga safari kuyazuru majen-go matukufu hajumuishwi na katazo hili na wala haingii katika maudhui hii. Maelezo haya ni kwa mujibu wa kadirio la kwanza.

Ama kwa kadirio la pili ni lazima safari zote za kidini ziwe zime-haramishwa isipikuwa safari za kwenda sehemu hizo tatu zilizotajwa, sawasawa safari hizo zitakuwa ni kwa ajili ya kuzuru msikiti au kuzuru sehemu nyinginezo.

## Kuzuru Makaburi

Lakini vielelezo na dalili zinaelekeza kwamba makadirio ya mwanzo ndiyo sahihi kama tutakubali kwamba njia ya upokezi wa hadithi hii ni sahihi.

Ama vielelezo vinavyoonyesha usahihi wa kadirio la kwanza ni kama ifuatavyo:

**Kwanza:** Kwa sababu misikiti iliyovuliwa ni mitatu, na uvuaji huo umo ndani ya maelezo husika, hivyo ni lazima kilichovua kiwe ni misikiti na wala si sehemu.<sup>39</sup>

**Pili:** Lau kama lengo lingekuwa ni kuzuia safari zote za kidini basi uvuaji huu, hapa usingesihi, kwani mwanadamu hufunga safari msimu wa Hijja kwa ajili ya kwenda “Arafa”, “Mash’aru” na “Mina”. Kwa hiyo kama safari za kidini zisizokuwa za misikiti mitatu zingekuwa ni haramu, basi ni kwa nini zinafungwa safari kwenda maeneo haya tuliyoyataja.

Hivi huu hauwi ushahidi kuwa Hadithi hii kwa namna hii amezuliwa Mtume (s.a.w.w.).

**Tatu:** Qur’ani Tukufu na Hadithi Tukufu vinaashiria kuwepo safari nyagine za kidini, na umekuja msukumo na mhimizo juu ya safari hizo, kama safari kwa ajili ya kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, kutafuta elimu, kuunga udugu, kuwatemebelea wazazi wawili na nyagine kama hizo.

Na mionganini mwa hayo ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

---

<sup>39</sup>. Laiti mtu akikwambia: Hakuja ila Zayd. Basi aliyevuliwa ndani ya sentensi hii ni mwanadamu au kaumku au mfano wa hayo, na wala haliwezi kuwa tamko la ujumla, kwa mfano kitu, kilichopo, ili iwe mwanadamu au kitu kingine

## Kuzuru Makaburi

﴿ وَمَا كَارَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا كَافَّةً فَلَوْلَا نَفَرَ مِنْ كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَائِفَةٌ لِّتَتَفَقَّهُوا فِي الدِّينِ وَلِيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ تَحْذَرُونَ ﴾  
١٢٢

“Wala haiwezekani kwa waumini kutoka wote, lakini kwa nini halitoki kundi katika kila taifa mionganini mwao kujielimisha vyema dini na kuwaonya watu wao watakapowarudia, ili wapate kujihadhari.”  
Tawba: 122.

Na kwa sababu ya Aya hii wafasiri wakubwa na wahakiki wa Hadithi wameitafsiri Hadithi hii kama tulivyoitafsiri sisi.

Al-Ghazali ndani ya kitabu chake *Ihyau-Ulumi* amesema: “Nayo ni kuwa mwanadamu asafiri kwa ajili ya ibada, ima ya Hija au Jihadi... Na katika jumla ya hayo inaingia kuzuru makaburi ya manabii (a.s.) na kuzuru makaburi ya maswahaba, tabiina, wanachuoni na mawalii wengine. Na kila ambaye (watu) hutabaruku kwake zama za uhai wake, basi watatabaruku kwa kumzuru baada ya kifo chake.

Na isharuhusiwa kufunga safari kwa lengo hili, na wala halizuiliki hili kutokana na kauli ya Mtume (s.a.w.w.) aliposema: “Haifungwi safari ila kwenda kwenye misikiti Mitatu: msikiti wangu huu na msikiti Mtukufu na msikiti wa mbali.” Kwa sababu Hadithi hii inahusu misikiti tu, kwani misikiti yote baada ya misikiti hii ni sawasawa katika ubora.

Na katika asili ya ubora hakuna tofauti baina ya kuzuru makaburi ya manabii, mawalii na wanachuoni, japokuwa katika daraja kuna tofauti kubwa kulingana na vyeo vyao mbele ya Mwenyezi Mungu.”<sup>40</sup>

<sup>40</sup> *Ihyau Ulumid-Dini* cha Al-Ghazali 2: 247, kitabu cha maadili ya safari, chapa ya Darul-Maarifah Beirut. *Al-Fatawa Al-Kubra* 2: 24.

## Kuzuru Makaburi

Hivyo kilichokatazwa katika Hadithi hii ni kufungwa safari kwenda kwenye misikiti yoyote isiyokuwa hiyo mitatu, wala haihusiki na safari ya kwenda kwenye misikiti au maeneo yaliyobarikiwa kwa lengo la kufanya ziara au kwa malengo mengine ya kidini.

Na linaonyeshwa hilo na zile riwaya walizozipokea waandishi wa *Sahih Sita* na Sunan kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akienda msikiti wa Quba hali akiwa juu ya kipando au kwa miguu, basi husali raka mbili msikitini.<sup>41</sup>

Ni lazima tujiulize: Vipi itawezekana kuwa haramu au ni jambo lililokatazwa, kufunga safari na kukata masafa kwa ajili ya kusimamisha Sala kwa iklasi ndani ya moja ya nyumba miuongoni mwa nyumba za Mwenyezi Mungu!!!! Na ikiwa kusalia msikitini ni Sunna basi kitangulizi cha Sunna ni Sunna vilevile.<sup>42</sup>

Na kuanzia hapa tunawakuta Mawahabi hawaoni ni haramu kulizuru kaburi la Mtume kwa kauli ya moja kwa moja - bali tunawakuta wanakiri asili ya ziara na ruhusa ya kufanya ziara, lakini safari kwa ajili ya ziara hiyo ndiyo wanayoihesabu kuwa ni haramu.

Muhammad bin Abdul-Wahabi amesema: “Ni Sunna kumzuru Mtume (s.a.w.w.) isipokuwa haifungwi safari ila kwa ajili ya kuzuru msikiti na kuswalia humo.”<sup>43</sup>

Ama Ibnu At-Taymiyyah yeye anasema: “Ama makaburi ya manabii na wachamungu si Sunna kuyaendea kwa lengo la kusalia kwenye

<sup>41</sup> *Sahih Muslim* 4: 127. rejea hadithi yenye maana hii ndani ya *Sahih Bukhari* 2: 76. As-Sunan An-Nasai iliyochapwa pamoja na ufanuzi wa As-Suyutwi 2: 37.

<sup>42</sup> Rejea *Al-Wahabiyyah Fil-Mizani* : 148 – 152. Uchunguzi juu ya Uwahabi.

<sup>43</sup> Risala ya pili miuongoni mwa risala za *Al-Hadiyyah As-Saniyyah* cha Muhammadi bin Abdul-Wahabi.

## Kuzuru Makaburi

makaburi hayo na kuomba dua kwenye kaburi la yeote miongoni mwa viongozi wa dini, bali hilo limekatazwa ndani ya hadithi sahihi, kama walivyosema wanachuoni zaidi ya mmoja, lakini inaruhusiwa kuyazuru makaburi kwa lengo la kuyaombea dua, kama Mtukufu Mtume alivyokuwa akiwazuru watu wa Baqii.<sup>44</sup>

Na Ibnu At-Taymiyyah anagawa ziara ya kaburi la Mtume kwenye namna tatu kwa kigezo cha nia na kusudio la msafiri:

Safari anayokusudia kuswalia kwenye msikiti wa Mtume, safari hii inaruhusiwa kwa ushahidi wa nassi na ijimai.

Safari anayokusudia kusafiri kwenda kwenye msikiti wake na kaburi lake (s.a.w.w.), safari hii kakusudia jambo la Sunna lililoruhusiwa kisheria kwa mujibu wa ijimai.

Safari ambayo hakusudii chochote ila ni kule kulizuru kaburi, hii ndiyo yenye utata. Malik na wanachuoni wengi wanaharamisha safari hii, na wengi miongoni mwa wanaoharamisha hawaruhusu kupunguza Swala katika safari hii. Na wengine wanaifanya ni safari iliyoruhusiwa, japokuwa si ya Sunna wala si ya wajibu kwa nadhiri.

Kwa ajili hii tunamkuta Al-Hafidhu Ad-Dhahabi ndani ya kitabu *Aalamu An-Nubalai* anamjibu Ibnu At-Taymiyyah kwa maelezo:

“Atakayesimama kwenye jiwe tukufu akiwa dhalili mwenye kutoa salamu na mwenye kumtakia Rehema Mtume wake, ana uzuri uliyoje! Atakuwa amefanya ziara nzuri, na amefanya udhalili na mapenzi bora, na amefanya ibada zaidi kuliko yule aliyemtakia rehema akiwa kwenye ardhi yake au ndani ya Swala yake.”

---

<sup>44.</sup> *Ar-Radu Alal-Akh'nai* cha Ibnu At-Taymiyyah. *Al-Fatawa Al-Kubra* cha Ibnu At-Taymiyyah 1: 118 – 122.

## Kuzuru Makaburi

Kwani mwenye kumzuru ana malipo ya ziara na malipo ya kumtakia rehema, na yule mwenye kumtakia rehema kwenye miji mingine ana malipo ya kumtakia rehema tu, hivyo atakayemtakia rehema mara moja, Mwenyezi Mungu humrehemu mara kumi.

Lakini yule atakayemzuru (s.a.w.w.) na akakosea maadili ya ziara au akalisujudia kaburi au akatenda kile kisichoruhusiwa kisheria, basi huyu ametenda jema na ovu, hivyo aelimishwe kwa upole, na Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mrehemevu.

Naapa kwa Mwenyezi Mungu mwisilamu hapatwi na hali ya kukereketwa, kilio, kuzibusu kuta na kuzidisha kilio ila ni kwa kuwa ni mwenye kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hivyo mapenzi yake ni kipimo na kitenganisho kati ya watu wa peponi na watu wa motoni.

Hivyo kulizuru kaburi lake ni mionganoni mwa ukuruba bora. Na iwapo tukikubali kuwa suala hilo la kufunga safari kwenda kwenye makaburi ya manabii na mawalii halijaruhusiwa kwa mjumuisho wa kauli ya (s.a.w.w.) : “Haifungwi safari ila kwenda kwenye misikiti mitatu....” basi kufunga safari kwenda kwenye kaburi la Mtume wetu kunalazimu kufunga safari kwenda kwenye msikiti wake, na suala hilo limeruhusiwa bila utata, kwani hawezi kufika kwenye chumba chake ila ni baada ya kuingia msikitini mwake.

Hivyo aanze kuusalimu msikiti, kisha amsalimu mwenye msikiti. Namuomba Mwenyezi Mungu aturuzuku sisi na ninyi kufanya hivyo. Amin.”<sup>45</sup>

Sheikh Shuaybu Al-Ar’nautwi amesema katika kuongezea maneno haya ya Ad-Dhahabi ndani ya kitabu *Siratu Aalamu An-Nubalai* kwa maelezo: “Mwandishi kwa ufanuzi huu amekusudia kumjibu Sheikh wake Ibnu

<sup>45</sup> *Siratu Aalamu An-Nubalai* cha Al-Hafidhu Ad-Dhahabi 4: 484.

## Kuzuru Makaburi

At-Taymiyyah ambaye anasema hairuhusiwi kufunga safari kwa lengo la kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume, na anaona kuwa Alhaji anawajibika kunuwia kuuzuru msikiti, kama alivyobainisha mahala husika.”

### **Saba: Ijimai juu ya ruhusa ya kuyazuru makaburi na kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)**

Waislamu wameafikiana kikauli na kivitendo juu ya kulizuru kaburi la Mtukufu Mtume, bali juu ya Sunna ya kuyazuru makaburi ya manabii na wachamungu na waumini wengine, na ruhusa yake kisheria inaunganishwa mionganoni mwa mambo ya dharura kwa waislamu, ukiachia mbali ijimai na sera yao iliyosimama juu ya hilo.

As-Samuhudi amenukuu kutoka kwa As-Subaki akisema: Iyadhu amesema: Kulizuru kaburi la Mtume (s.a.w.w.) ni Sunna iliyopo kati ya Waislamu, na imesimama ijimai juu ya hilo, na fadhila zake zimehimizwa.<sup>46</sup>

As-Sabki amesema: “Wanachuoni wameafikiana juu ya Sunna ya kuyazuru makaburi kwa wanaume, kama alivyoeleza An-Nawawi, bali baadhi ya Dhahiriyyah<sup>47</sup> wamesema ni wajibu na wakatofautiana kuhusu wanawake. Na kaburi la Mtukufu Mtume limetofautishwa kwa dalili maalumu, kwa ajili hii nasema kuwa: Hakuna tofauti kati ya wanaume na wanawake.<sup>48</sup>

### **Maneno ya wanachuoni juu ya ruhusa ya kuzuru makaburi**

Zifuatazo ni baadhi ya sentensi za kauli za wanachuoni zenyenye kubainisha ruhusa ya kuzuru makaburi, bali ni Sunna kwa wanachuoni wote:

46. *As-Shafa cha Kadhi Iyadhi* 2: 83.

47. Hili ni kundi la watu wanaohukumu na kutoa fatuwa kulingana na dhahiri ya matamko bila kujali kanun I na misingi mingine ya kilunga au kitaaluma (Mtarjumi).

48. *Shifau As-Suqami* cha As-Sabki: 69, 70, chapa ya Istambuli 1318 A.H.

## Kuzuru Makaburi

Imam Abu Abdullah Muhammad bin Idirisa As-Shafi amesema: “Wala si vibaya kuyazuru makaburi, lakini hayasemwi maneno machafu mbele yake, kwa mfano kulia kwa kuona umepatwa na balaa au kwa kukata tamaa, utakapofanya ziara muombee maiti msamaha na moyo wako ulainike.”<sup>49</sup>

Al-Hakimu anasema: “Nimemaliza kuhimiza kuyazuru makaburi kwa lengo la kushiriki katika kutoa motisha, na ili aliyebahili kwa dhambi yake ajue kuwa kuyazuru ni Sunna iliyothibiti kisheria.”<sup>50</sup>

Sheikh Zaynud-Dini mashuhuri kwa jina la Ibnu Najimu Al-Misriyu amesema: “Wala si vibaya kuyazuru makaburi na kuwaombea dua wafu. Na ndani ya kitabu Al-Mujtaba ametamka wazi kuwa ni Sunna, na ikase-mekana kuwa: Ni haramu kwa wanawake, lakini sahihi zaidi ni kuwa ruhusa imethibiti kwa wote wawili.”<sup>51</sup>

Mansur Ali Nasifu amesema: “Amri ya kuyazuru makaburi ni amri ya Sunna kwa Masunni.”<sup>52</sup>

Ibnu Hazmi amesema: “Na ni Sunna kuyazuru makaburi, na kitendo hicho ni faradhi angalau mara moja, imesihi ruhusa ya kuyazuru makaburi kuto-ka kwa Mama wa waumini, Ibnu Umar na wengine. Na katazo la kitendo hicho limepokewa kutoka kwa Umar, lakini halijasihi.”<sup>53</sup>

Abu Hamid Al-Ghazali amesema: “Kuyazuru makaburi ni Sunna kwa wote, kwa ajili ya kujikumbusha na kujifunza, na kuyazuru makaburi ya wachamungu ni Sunna kwa ajili ya kutabaruku na kujifunza.”<sup>54</sup>

49. *Maarifatu As-Sunan Wal-Athari* cha Shafi 3: 203, mlango wa kuyazuru makaburi.

50. *Mustadrak Al-Hakimu* 1: 377.

51. *Al-Bahru Ar-Raiqu fi Sharhi Kanzud-Daqaiqi* 2: 195.

52. *At-Taji Lil-Jamii Lil-Usuli* 1: 381.

53. *Al-Mahali* 5: 160, suala la 600.

54. *Ihyaoul-Ulumi* 4: 521.

## Kuzuru Makaburi

Abdur-Rahmani Al-Jazayriyu amesema: "Kuyazuru makaburi ni Sunna kwa ajili ya kuwaidhika na kujikumbusha Akhera, na inasisitizwa siku ya Ijumaa na siku moja kabla yake na siku moja baada yake, hiyo ni kwa wafuasi wa Hanafi na Malik. Ama wafasi wa Shafi na Hambali wamekhali ifu hilo:

Hambali wamesema: Haisisitizwi kufanya ziara ndani ya siku hii kuliko ile.

Shafi wamesema: Inasisitizwa siku ya Alhamisi kuanzia alasiri mpaka wakati wa kuchomoza jua siku ya Jumamosi, na hii ndio kauli bora kwa wafuasi wa Malik.<sup>55</sup>

Madhehebu ya Ahlul-Bait imesema: Sunna hiyo ya kuyazuru makaburi inasisitizwa siku ya Jumatatu na asubuhi ya siku ya Jumamosi, hiyo ni kumfuata Mtume,<sup>56</sup> kwani ye ye aliкуwa akitoka na baadhi ya Sahaba zake kila jioni ya Alhamisi kwenda Baqii ya Madina, akifika anasema:

"السلام عليكم يا أهل الديار"

"Amani iwe juu yenu enyi watu wa makazi haya (mara tatu),

رحمكم الله"

Mwenyezi Mungu awarehemu (mara tatu)."<sup>57</sup>

Sasa ni jinsi gani Mashi'a wanazuru makaburi ya Maimamu wao?

Na je, kuwazuru Maimamu kunapelekea maadili mabaya yanayopingana na dini?

Au kwenyewe kunaotesha roho ya shirki dhidi ya Mwenyezi Mungu?

<sup>55</sup> *Al-Fiqhu Alal-Madhahibi Al-Arbaah* 1: 540 hitimisho kuhusu kuyazuru makaburi.

<sup>56</sup> *Jawharul-Kalami* 4: 321, kitabu cha tohara, Sunna ya kuyazuru makaburi.

<sup>57</sup> *Wasailu Shi'a* cha Huru Al-Amili 3: 223, hadithi ya 3467.

## Kuzuru Makaburi

Jibu: Kuna mifano mbalimbali ya ziyara<sup>58</sup> ambazo Shi'a Imamia wamezirithi kutoka kwa Maimamu wa kizazi cha Mtume (a.s.), na ambazo zinaendana na munasaba husika na yule muhusika anayefanyiwa ziara.

Anayefuatilia na kuchunguza mifano hiyo ya ziara hizo zenyе kutegeme-wa kwa namna maalumu atazikuta kuwa zina thamani kubwa katika kuotesha imani ya tawhidi na kuipandikiza ndani ya akili na nafsi ya mwenye kuzuru, vilevile zenyewe ni ibada inayosaidia kuotesha roho ya kumwamini Mwenyezi Mungu na kushikamana Naye.

Ufuatao ni mfano mmoja tu mionganoni mwa ziyara hizo, nayo ni ziyara ijulikanayo kwa jina la Ziyara ya Mwaminifu wa Mwenyezi Mungu, nayo ni ziyara iliyojaa maana yenye nguvu, fikira salama, lugha ya tawhidi, maelezo ya moyo na kuamsha hisia, na zenyewe ni ubao wa kudumu unaowapa nguvu Shi'a Imamia na hivyo wanauhifadhi moyoni, hayo ni kutoekana na thamani unayoibeba ziyara hiyo katika kumfuniganisha mwislamu kati yake na Mwenyezi Mungu Mtukufu na mawali wake.

Kwa ajili hiyo mwandishi wa kitabu *Mafatihul-Jinani* ameizingatia kuwa ni mionganoni mwa ziyara ambazo ziko katika hadhi ya juu. Ama Al-Majlisi mwandishi wa kitabu *Biharul-Anwaar* amesema: Yenyewe ni mionganoni mwa ziyara bora mno upande wa njia ya upokezi na matamko, na zenyewe imepokewa kutoka kwa Jabir kutoka kwa Imamu Al-Baqir (a.s.), Imamu Zainul-Abidina alimzuru babu yake kiongozi wa waumini Ali bin Abu Twalibi kwa kutumia ziyara hii.<sup>59</sup>

Na yafuatayo ni maneno ya ziyara hiyo:

<sup>58</sup> Tamko Ziyara hapa linamaanisha yale maneno ayasemayo mtu mwenye kufanya ziara wakati wa kufanya ziara hiyo. Hivyo kuna neno: Ziara ambalo humaanisha kile kitendo kizima cha ibada hii tukufu, na kuna neno Ziyara ambalo humaanisha maneno hayo husika (**Mtarjumi**).

<sup>59</sup> Rejea kitabu *Mafatihul-Jinani* cha kiarabu: 350.

## Kuzuru Makaburi

السلام عليك يا أمين الله في أرضه وحجته على عباده، السلام عليك  
 يا أمير المؤمنين أشهد أنك جاهدت في الله حق جهاده،  
 وعملت بكتابه واتبعك سنتن نبيه صلى الله عليه  
 وأله حتى دعاك الله إلى جواره فقبضك إليه باختياره وأنزل  
 أعداءك الحجة مع مالك من الحجج بالغة  
 على جميع خلقه

اللهم فاجعل نفسى مطمئنة بقدرك، راضية بقضائك، مولعة  
 بذكرك ودعائك، محبة لصفوة أوليائك، محبوبة فى أرضك وسمائك،  
 صابرۃ على نزول بلائك، شاکرۃ لفوافض نعمائك، ذاکرۃ  
 لسوابیغ آلانك، مشتاقۃ إلى فرحة لقائك، متزوڈة التقوی ليوم جزانك،  
 مستنیة بسنن أوليائك، مفارقة لأخلاق أعدائك، مشغولة عن  
 الدنيا بحمدك وثنائك.

اللهم إن قلوب المختفين إليك والهبة، وسبل الراغبين إليك شارعة،  
 وأعلام القاصدين إليك واضحة، وأفندة العارفين منك فازعة،  
 وأصوات الداعين إليك صاعدة، وأبواب الإجابة لهم مفتوحة،  
 ودعوة من ناجاك مستجابة، وتوبة من أتاب إليك مقبولة،  
 وعبرة من بكى من خوفك مرحومة، والإغاثة لمن استغاث  
 بك موجودة، والإعانة لمن استعن بك مبذولة، وعداتك  
 لعبادك منجزة، وزلل من استقالك مقالة، وأعمال العاملين لديك  
 محفوظة، وأرزاقك إلى الخالق من لدنك نازلة، وعوند المزيد  
 إليهم واصلة، وذنوب المستغفرين مغفرة، وحوانج خلقك  
 عندك مقضية، وجوانز السائلين عندك موفرة، وعوند  
 المزيد متواترة، وموائد المستطعمين معدة، ومنناه  
 الظماء متربعة.

اللهم فاستجب دعائي واقبل ثاني واجمع بيني وبين  
 أوليائي بحق محمد و علي و فاطمة والحسن والحسين  
 إنك ولي نعمائي ومنتهى مناي، وغاية رجائى في منقلبي

وثم واي

## Kuzuru Makaburi

“Amani iwe juu yako ewe mwaminifu wa Mwenyezi Mungu ndani ya ardhi Yake na hoja Yake juu waja Wake. Amani iwe juu yako ewe kiongozi wa waumini.

“Nashuhudia kwamba wewe ulipigana katika njia ya Mwenyezi Mungu jihadi ya kweli, ukatenda kwa mujibu wa kitabu chake na ukafuata Sunna za Mtume wake (s.a.w.w.) mpaka pale Mwenyezi Mungu alipokuita karibu Yake, basi akakuchukua Kwake kwa uchaguzi Wake na akawashinda maadui Zake kwa hoja, pamoja na hoja nyin-gi kali ulizonazo juu ya viumbe Wake wote.

“Ewe Mwenyezi Mungu, ifanye nafsi yangu iwe tulivu kwa uwezo Wako, yenye kuridhia kadirio Lako, yenye kung’ang’ania utajo Wako na dua Kwako, kwa ajili ya kumpenda mteule bora kati ya Mawalii Wako, mwenye kupendwa ndani ya ardhi Yako na mbingu Yako.

“Yenye kuvumilia mteremko wa balaa Yako, yenye kushukuru fadhila za neema Zako, yenye kukumbuka raha za neema Zako, yenye shauku na furaha ya kukutana na Wewe, yenye kujiandalia uchaji kwa ajili ya Siku ya Malipo Yako, yenye kufuata mwenendo wa mawalii Wako, yenye kujitenga na maadili ya adui Zako, yenye kujishughulisha dhidi ya dunia kwa kukuhimidi na kukusifu.

“Ewe Mwenyezi Mungu, hakika nyoyo za wenye matumaini ya kuja Kwako ni zenye kutahayari, na njia za wenye raghba ya kuja Kwako ni zenye kubainika, na alama za wenye kukusudia kuja Kwako ziko wazi, na vifua vya wenye kukujua ni vyenye kutetemeka, na sauti za wenye kukuomba ni zenye kupanda, na milango ya

## Kuzuru Makaburi

kuwajibu ni yenyе kufunguka, na maombi ya mwenye kukunong'oneza ni yenyе kujibиwa.

“Na toba ya mwenye kurejea Kwako ni yenyе kukubaliwa, na machozi ya mwenye kulia kwa ajili ya kukuhofia ni yenyе kuhurumiwa, na msaada wa mwenye kukuomba msaada upo, na usaidizi wa mwenye kukuomba usaidizi ni wenyе kutolewa, na ahadi Yako kwa waja Wako ni yenyе kutekelezwa, na utelezi wa aliyekuomba punguzo ni wenyе kupunguzwa, na matendo ya wenyе kutenda ni yenyе kuhifadhiwa Kwako.

“Riziki za viumbe Wako ni zenyе kuteremka kutoka Kwako, na nyongeza za wema ni zenyе kuwafikia, na dhambi za wenyе kuomba msamaha ni zenyе kusamehewa, na haja za viumbe Wako ni zenyе kukidhiwa Kwako, na zawadi za wenyе kuomba ni zenyе kujaa Kwako, na nyongeza za wema ni zenyе kuendelea, na meza za wenyе kuomba chakula ni zenyе kuandaliwa na maeneo ya kunya wea wenyе kiu ni yenyе kufurika.

“Ewe Mwenyezi Mungu, jibu dua yangu, ukubali sifa zangu na unikusanye mimi na watawala wangu kwa haki ya Muhammad, Ali, Fatima, Hasan na Husein, hakika wewe ni msimamizi wa neema yangu na mwisho wa matamanio yangu, na ukingo wa matarajio yangu katika marejeo yangu na makazi yangu.”

**Ndani ya kitabu *Kamilu Ziyarah*, mwishoni imeongezwa:**

## Kuzuru Makaburi

"أَنْتَ إِلَهِي وَسَيِّدِي وَمُوْلَايِ، اغْفِرْ لِأُولِيَّانَا، وَكُفْ عَنْ أَعْدَاءِنَا وَاسْغُلْهُمْ عَنْ أَذَانَا، وَأَظْهِرْ كَلْمَةَ الْحَقِّ وَاجْعُلْهَا الْعُلِيَا، وَادْحُضْ كَلْمَةَ الْبَاطِلِ وَاجْعُلْهَا السُّفْلَى، إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ."

"Ewe Mungu wangu, Wewe ndio Bwana wangu na Mtawala wangu, wasamehe watawala wetu, na wazuie maadui zetu dhidi yetu na washughulishe dhidi ya kutuudhi, na lidhahirishe neno la haki na ulifanye la juu, na liondoe neno la batili na ulifanye la chini, hakika Wewe ni Muweza juu ya kila kitu."

## MUHTASARI WA UCHUNGUZI

Hakika kitendo cha kuzuru makaburi hakikomei kwenye jamii ya kidini tu, bali chenyewe kinajumuisha jamii za aina zote, na sheria tukufu imekipitisha, bali imekitilia umuhimu, na kilichothibiti kutoka kwa Mtukufu Mtume ni kuwa yeye alikuwa akizuru makaburi ya wafu, kama vile kaburi la mama yake mzazi na makaburi ya wafu huko Baqii.

Ama sera ya waislamu iliendelea kwa kuzuru makaburi ya wafu mionganoni mwa manabii na wachamungu, zama za uhai wa Mtume na baada ya kifo chake na mpaka leo hii.

Kisha hakika kitendo cha kuzuru kaburi la Mtukufu Mtume kimethibiti kisheria kwa dalili za Qur'an na Hadithi Tukufu, na chenyewe hakihu su zama za uhai wa Mtukufu Mtume tu, wala dua yake tu, bali kinaendelea mpaka baada ya kifo chake na kumuomba kwa maombi mbalimbali.

Wala kauli ya Ibnu At-Taymiyyah kuhusu kuharamisha kuzuru kaburi la Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) haiko sawa kwa kuwa inapingana na Qur'an Tukufu, Hadithi Tukufu, sera ya waislamu na ijimai ya wanachuoni waliyokubaliana kuwa ni Sunna.

Kimetarjumiwa na:

Hemedi Lubumba Selemani (Lipumba)

## Kuzuru Makaburi

### **ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:**

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza mpaka Ishirini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhangaa wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi

## Kuzuru Makaburi

25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeesi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba' Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto

## Kuzuru Makaburi

54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatoo
67. Tujifunze Misingi Ya Dini
68. Sala ni Nguzo ya Dini
69. Mikesha Ya Peshawar
70. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
71. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
72. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
73. Liqaa-u-llaah
74. Muhammad (s) Mtume wa Allah
75. Amani na Jihadi Katika Uislamu
76. Uislamu Ulienea Vipi?
77. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
78. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)

## Kuzuru Makaburi

### BACK COVER

Kuzuru makaburi ni desturi iliyokuwepo tangu wakati wa Mtukufu Mtume (s.a.w.). Desturi hii iliendelezwa na makhalfa na Maimamu (a.s.) katika zama zao mpaka mwanzoni mwa karne ya 13 Hijria wakati madhehebu ya Uwahabi ilipozuka, ndipo masheikh wa Kiwahabi walipoanza kuzunguka katika miji ya Waislamu na kuwakataza Waislamu kuzuru makaburi, wakisemi eti ni shirki, bidaa na haramu.

Masheikh hao wa Kiwahabi waliilazimisha itikadi yao hii kwa Waislamu, na hatimaye wakafikia kuyavunja makaburi ya wanavyuoni wa Kiislamu na wajukuu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.) hapo *Jannatu'l-Baqii* (Madina) katika mwaka wa 1343 Hijria, na makaburi ya *Jannatu'l-Mualla* (Makka). Hali hii imeendelea mpaka imefikia huku kwetu Afrika ya Mashariki. Ziko taarifa kutoka sehemu mbali mbali za eneo hili la Afrika za kuvunjwa kwa makaburi ya Waislamu kwa amri ya masheikh wa Kiwahabi.

Kutokana na hali hii, mwandishi wa kitabu hiki ameamua kuiangalia upya historia ya Uislamu na kutoa dalili kutoka Qur'ani Tukufu na Sunna na akaonesha wazi kabisa kwamba kuzuru makaburi ni desturi iliyokuwepo tangu zama za Mtukufu Mtume (s. a. w.). Na mwenendo huo ukafuatwa na makhalfa na masahaba baada ya Mtume. Kwa hivyo, kuzuru makaburi si shirki, si haramu wala si bidaa kama wanavyoitakidi kimakosa masheikh hao wa Kiwahabi.

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**

**Al-Itrah Foundation**

**P. O. Box 19701. Dar es Salaam, Tanzania**

**Simu: +255 22 2110640**

**Simu/Fax: +255 22 2127555**

**Email: alitrah@raha.com**

**Website: www.alitrah.org**

**Online: www.alitrah.info**